


MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

MALALAMIKO NAMBA. GA.71/135/NZ/2021/10

ALBERT A. TEMU NA ELIOT D. LYATUU
KWA NIABA YA WAKAZI WA ENEO LA
OLD MOSHI MAHOMAWALALAMIKAJI

DHIDI YA

SHIRIKA LA UGAVI UMEME TANZANIA (TANESCO).....MLALAMIKIWA



1.0 Maelezo ya Awali:

Mnamo tarehe 3 Septemba 2021, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji "EWURA" ("Mamlaka") ilipokea malalamiko kutoka kwa Bw. Albert A. Temu na Bw. Eliot D. Lyatuu wa eneo la Old Moshi Mahoma, Kata ya Old Moshi Wilaya ya Moshi Vijijini, Mkoa wa Kilimanjaro ("Walalamikaji") wakilalamikia Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania ("TANESCO") ("Mlalamikiwa"). Walalamikaji wamelalamikia huduma duni kama vile kutoshughulikiwa malalamiko yao ya kubadilisha nguzo chakavu, nyaya zisizo na maganda na kutokukatwa mti inayogusa nyaya kitu ambacho ni hatarishi katika makazi yao.

Walalamikaji wanaeleza kwamba nguzo ya umeme katika eneo lao imeoza na kulalia chini na hivyo kusababisha nyaya kushuka chini sana. Pia Walalamikaji wanaripoti kwamba nyaya za umeme sizizo na maganda

zinagusana zenyewe na wakati mwingine zinagusa matawi ya miti kitu ambacho ni hatarishi katika makazi yao. Walalamikaji wanadai kuwa wamewahi kufikisha malalamiko awali kwa Mlalamikiwa lakini hakuna hatua iliyochukuliwa, ndipo tarehe 9 Septemba 2020 walipeleka barua ya malalamiko lakini hadi sasa hajafanya hatua yoyote ya utatuzi.

Walaamikaji walileta malalamiko yao EWURA na kuiomba Mamlaka imuamuru Mlalamikiwa kufanya yafuatayo:

- (a) abadilishe nyaya pamoja na nguzo chakavu; na
- (b) akate matawi ya miti ambayo nyaya za umeme zinapita katikati ili kuondoa hatari inayoweza kutokea.

Baada ya kupokea malalamiko ya Walalamikaji, Mamlaka (EWURA) tarehe 9 Septemba, 2021 ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) ya Kanuni za EWURA za Taratibu za Kutatua Migogoro T. S. 428/2020 '*Rule 6 (1) of the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Complaints Handling Procedure) Rules, GN No. 428/2020*'.

Mnamo tarehe 30 Septemba 2021, Mlalamikiwa alileta utetezi wake akaieleza Mamlaka kwamba Shirika linaomba radhi kukawia kufanya utekelezaji wa ombi la Walalamikaji kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wao. Mlalamikaji ameeleza kwamba Shirika limepanga kutekeleza nafuu zilizombwa na Walalamikaji ndani ya siku saba toka tarehe ya utetezi huu. Mlalamikiwa alihitimisha kwa kueleza kwamba wanatambua usumbufu walioupata wakazi wa eneo la Old Moshi Mahoma kwa kipindi chote tangu walipowasilisha malalamiko yao, hivyo wanaahidi kutekeleza utatuzi ndani ya muda uliotajwa kwenye kipengele cha utetezi.

Kikao cha usuluhishi baina ya pande zote mbili kilifanyika tarehe 13 Oktoba 2021 katika Ukumbi wa Hoteli ya Uhuru Mjini Moshi, Kilimanjaro. Katika kikao cha usuluhishi, Walalamikaji walikiri kwamba Mlalamikiwa ameshaweka nguzo mpya mbili na kufunga nyaya zenyewe maganda (*insulated conductors*) kwenye makazi yao. Mlalamikiwa alieleza kwamba kwa mujibu wa taratibu za Shirika, Walalamikaji ndio wenye jukumu la kukata miti ambayo nyaya za

umeme mdogo (*Low Tension*) zimepita katikati. Mlalamikiwa aliongeza kueleza kwamba kibali cha kukata miti kinatolewa Ofisi za Mkuu wa Wilaya na Shirika litawajibika kutoa huduma ya kuhakikisha usalama unakuwepo wakati wa ukataji wa mti huo.

Mwishoni, muafaka kati ya Mlalamikaji na Mlalamikiwa ulifikiwa kwa makubaliano yafuatayo:

- (a) Mlalamikaji na Walalamikiwa watashirikiana kukamilisha taratibu na vibali vyta kukata mti ambao nyaya za umeme mdogo (*Low Tension*) zimepita katikati; na
- (b) Mlalamikiwa atawapatia Walalamikaji huduma ya kushusha nyaya za umeme kupisha ukataji wa mti muda wowote kati ya tarehe 18 na 31 Oktoba 2021.

Makubaliano haya yamewekwa kwenye maandishi kama inavyoainishwa kwenye kanuni ya 14(4) ya Kanuni za Taratibu za Kutatua Migogoro T. S. 428/2020 '*Rule 14(4) of the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Complaints Handling Procedure) Rules, GN No. 428/2020*' na kama inavyoanishwa kwenye fomu ya makubaliano.

2.0 Makubaliano

Pande zote mbili zimefikia muafaka kuwa:

- (a) Mlalamikaji na Walalamikiwa watashirikiana kukamilisha taratibu na vibali vyta kukata mti chakavu na hatarishi ambao nyaya za umeme mdogo (*Low Tension*) zimepita katikati; na
- (b) Mlalamikiwa atawapatia Walalamikaji huduma ya kushusha nyaya za umeme kupisha ukataji wa mti muda wowote kati ya tarehe 18 na 31 Oktoba 2021.

Kwa mujibu wa kifungu cha 14(5) cha Kanuni za Taratibu za Kutatua Migogoro T. S. 428/2020 makubaliano haya yameandikishwa kama Tuzo ya Mamlaka. Kila upande utabeba gharama zake katika shauri hili.

IMETOLEWA KWA LAKIRI ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Dodoma tarehe 3 Novemba, 2021.



.....
**KAPWETE LEAH JOHN
KATIBU WA BODI**